

MABWANA, SISI

TUNATAKA KUMWONA YESU



Baba wa Mbinguni, tunaukomboa tu wakati sasa mpaka Wewe utakapokuja. Ule ufufuo mkuu ambao tumeufurahia vizuri sana, ambao ulienea nchini kote na kila mahali ulimwenguni kote, mpaka mioto ya ufufuo imewaka katika kila taifa chini ya mbingu. Kila mahali ulimwenguni, wakati huu, kuna ibada zenye nguvu za uponyaji zinazoendelea, mchana kutwa na usiku kucha, kila mahali ulimwenguni, zilizoanza tangu miaka michache iliyopita. Ni watu wanyenyekevu tu wakitoka, wakiadini, na kuleta ufufuo. Baba wa Mbinguni, sasa tunaokota masazo katika miji yetu na kila mahali nchini mwetu. Je! kuna wengine, Bwana, ambao bado hawajaingia? Kama wapo, Mungu wetu, tunaomba ya kwamba Wewe utawaleta. Kama kuna nafsi zo zote hapa Dallas, ambazo zinaweza kukombolewa, zijalie, Bwana, ya kwamba kwa namna fulani, kwa njia fulani, utazipata katika mkutano huu.

² Sisi hatujaliwi sana kati ya watu wa ulimwengu, nasi tunalitarajia jambo hilo. Lakini wakati Bwana wetu alipokuja duniani, wala Yeye hakujaliwa sana. Lakini kulikuweco na mamilioni ulimwenguni wakati huo, na ni wachache tu waliomsikia. Lakini wale wote waliokuwa wamekusudiwa Uzima, walimsikia Yeye. Naomba, Mungu, kwa uaminifu, ya kwamba Wewe utawapa, usiku wa leo na kwenye mkutano, wale wote waliosalia hapa Dallas bila Muhuri wa Mungu kwenye vipaji vya nyuso zao, wajalie ili kwamba waingie, wajazwe vizuri sana na Roho Mtakatifu.

³ Naomba ya kwamba utawaponya wagonjwa wote na wanaoteseka kote kote humu nchini kote, walio na imani.

⁴ Mbariki maskini ndugu yetu mwema, Ndugu Grant. Loo, kumwona akiwa na nguvu zaidi! Maskini mtu huyo aliathirika afya yake, akiwa amesimama papo hapo chini, kwenye mistari ya maombi, katika uaminifu mkubwa, na moyo wangu unampenda. Nina furaha kuona, Bwana, vya kwamba umembariki wa ajabu sana. Mkono Wako wa huruma na uwe juu yake, na wote wale waliomo nchini humu wanaokupenda na wanangojea Kuja Kwako.

⁵ Bariki Neno Lako. Na, Baba, tunaomba ya kwamba Yesu Mwenyewe atatuja, katika hali ha—halisi, katika njia halisi sana hata hakuna hata mmoja wetu atakayeshindwa kumwona Yeye, na jalia wote ambao Wewe umewakusudia Uzima walipokee. Jalia wale walio wagonjwa wampokee Yeye,

na wajalie waponywe kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina.

⁶ Sasa tutajaribu kumaliza ibada kati ya saa tatu na saa tatu na nusu, kwa sababu ya u—umati wa watu, na kwa ili mweze kurudi kesho usiku. Ni mkutano tu mdogo wa kawaida, usiku wa leo, ninataka kuchukua Andiko ambalo nimelisoma mara nyingi. Na limeninii . . .

⁷ Kuna watu hapa ambao hawajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano hii? Inueni mikono yenu, hebu tuone. Loo, jamani, hiyo ni karibu asilimia themanini ama tisini ya —ya jengo hili, ama watu waliomo kwenye jengo hili, hawajahudhuria mkutano. Nina furaha kuwa nanyi kwa mara hii ya kwanza.

⁸ Sasa, mtu ye yote anajua ya kwamba hakuna mtu anayeweza kumponya mwingine. Hata hakuna daktari anayeweza kukuponya. Uponyaji ni wa Mungu. “Mimi ni Bwana anayewaponya magonjwa yenu yote.” Hakuna daktari atakayekwambia ya kwamba ana dawa zitakazokuponya. Kama akikwambia hivyo, anakudanganya.

⁹ Kwa sababu, Mayo Brothers, kwenye mahojiano hivi majuzi . . . Wakati maskini huyu Donny Morton alipoponywa huko Canada, ambaye Mayo walikuwa wamemkatia tamaa, jambo ambalo lilitukia kwenye Pwani ya Magharibi. Mliliona jambo hilo kwenye Reader’s Digest. Walikuwa wameniita kule kwa mahojiano, nao wakasema, “Sisi hatudai kuwa waponyaji, Ndugu Branham, tunadai tu kuyasaidia maumbile.”

¹⁰ Kuna Mponyaji mmoja, huyo ni Mungu. Mungu ndiye tu anayeweza kujenga seli, kufanya uhai, kwa hiyo mwanadamu hana uwezo wa kufanya jambo hilo. Daktari anaweza kuuweka mfupa vizuri; ama akupe dawa ya kuua virusi, ambayo ameuweka kiasi fulani ndani yake, na topozi kuifanya isikuue, na kuua hivyo virusi na kadhalika. Yeye anaweza kufanya hivyo. Lakini ile nyama ambayo imeharibiwa, ama ule mfupa ambao umevunjwa, kile kidole tumbo ambacho kimetolewa, hicho kidole tumbo, yeye hawezi kukiponya hicho. Inahitaji Mungu. Mungu huponya. Mwanadamu anaweza kuondoa kitu fulani kinachousababisha, kama inawezekana kuondoa kiungo hicho, anaweza kukikata kitoke, akate mishipa ya damu na akivute kitu hicho kuiondoa hiyo, ama kiungo hicho, hiyo ni seli mbaya, kama vile kivimbe, kansa, ama cho chote kile. Kama anaweza kukipata, anaweza kukitoa. Lakini kuponya, yeye hawezi, na atakwambia jambo hilo.

¹¹ Na, sasa, kuponya ni kwa Mungu peke yake. Mungu peke yake ametununulia uponyaji wetu. Ni juu yetu sisi kufanya jambo lo lote tutakalo, katika maisha yetu, na kwa kila njia ambayo Mungu ametupa, kwa ajili ya uponyaji wetu, lakini Mungu ndiye anayeponya. Kama Mungu akikuita kwenda Nyumbani, usiku wa leo, hakuna dawa za kutosha ulimwenguni

zitakazokuweka hapa. Hakuna kitu kitakachokuweka hapa. Na kama akiamua kwamba ukae duniani, haidhuru ni madaktari wangapi wanaosema utaaga dunia usiku huu, hutakufa. Kwa hiyo yote ni juu ya Mungu.

¹² Mungu ni Uzima, Uzima wa Milele. “Hapo Mwanzo alikuweko Mungu.” Yeye hakuwa Mungu wakati huo, kwa maana *mungu*, neno la Kiingereza *mungu*, linamaanisha “kitu cha kuabudiwa,” na hakukuweko na kitu cho chote ila Yeye. Yeye alikuwa ni wa Milele, Yule tu wa Milele. Hapakuwepo na mwezi, hakuna nyota, hakuna Malaika, hakuna kitu. Lakini ndani ya Mwenye Uhai huyu, ambaye tunamwita “Mungu Baba yetu,” mlikuwemo na sifa. Ndani Yake mlikuwemo na sifa za kuwa Baba, ndani Yake mlikuwemo sifa za kuwa Mungu, ndani Yake mlikuwemo sifa za kuwa Mwana, ndani Yake mlikuwemo na sifa za kuwa Mwokozi, ndani Yake mlikuwemo na sifa za kuwa mponyaji, na mambo haya yote tunayoona sasa yanaonyesha tu sifa Zake.

¹³ Sasa, kama ulikuwa katika mawazo Yake, hapo mwanzo, kama una Uzima wa Milele, kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele. Uzima wa Milele haukuwa na mwanzo wala hauna mwisho. Kwa hiyo kama una Uzima wa Milele, ulikuwa sifa ya mawazo ya Mungu kabla hapajakuweko na cho chote kile ila Yeye.

¹⁴ Umbo lako, sura yako, na kile ulicho ndani yako sasa, ni negativu tu, unapofikia umri wa miaka ishirini hivi, ishirini na miwili. Ulikuwa negativu, na kifo kinaisafisha hiyo picha iwe halisi, “ili kwamba wakati maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tuna moja inayongoja tayari.” Mnaona?

¹⁵ Huu, ni wonyesho tu, sasa unaonyesha yale yanayofanywa. Kama vile Mungu alivyofanyika Mungu wakati alipowaumba Malaika. Yeye alifanyika Mwana alipomuumba Kristo Yesu. Alifanyika Mwokozi wakati Yesu alipokufa. Alifanyika mponya wakati Yeye “Apojeruhiwa kwa makosa yetu, kwa mapigo Yake sisi tulipona.” Mnaona?

¹⁶ Mambo yote haya yote ni sifa za Mungu, ili kwamba tu hapo mwishoni—mwisho, Biblia ilisema, Yesu alisema, “Mtajua ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani Yangu.” Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu. Ni Mungu akigeuka kuwa anayeweza kushikika. Mke wako mwenyewe, wewe na mume wako, ni kivuli tu, negativu ya Mungu na Mke Wake, Kanisa. Mnaona, ni sifa tu za Mungu zikionyeshwa katika vivuli na mifano, kama vile Agano la Kale lilivyokuwa kwa lile Jipya. Mnaona? Ndipo mwishowe, yote inaishia, Mungu agusikaye. Mungu katika Kristo, anayeweza kushikika, akafanyika mwili, akakaa kwetu. Na katika ule Utawala mkuu wa Miaka elfu unaokuja, Mungu katika umbo la Kristo, anaketi kwenye kiti

cha enzi cha Daudi; na Kanisa, Bibi-arusi Wake, Mume na Mke pamoja.

¹⁷ Mbona, ni ninii sana, inatosha kuuwasha moto moyo wa mwamini; katika saa hhizi kuu tunayoishi, wakati matumaini yote na mataifa, na cho chote kile, vinatuharibikia, chini yetu, tuna Ufalme. Tumebatizwa katika Ufalme huu.

¹⁸ Sasa tutachukua Ujumbe huu mdogo wa kawaida, usiku wa leo, ili kutangulia jambo ninalotaka muone katika mikutano. Tunasoma katika, samahani, katika Yohana Mtakatifu sura ya 12 na aya ya 20. Na ki—kiini chetu, bado, tangu mwanzo, ni kama ilivyo usiku wa leo, na kwenye vitabu vyote vyetu na kila kitu, Waebrania 13:8, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

Sasa palikuwa na Wayahudi kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu:

Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida . . . wakamwomba, wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.

¹⁹ Sasa hilo ndilo swali tunaloliuliza usiku wa leo. Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na hawa Wayunani, Mataifa, waliomba wapate kumwona Yeye, nao wakaruhusiwa kufanya hivyo na mmoja wa watumishi Wake, na kama Yeye angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kwa nini hatuwezi kumwona usiku wa leo? Mnaona? *Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu.*

²⁰ Sasa mimi nina hakika, kwa mwamini ye yote, lingekuwa ndilo jambo la kufurahisha sana la moyoni mwake, thibitisho la imani yake, ya kwamba kama yeye angeweza kweli kuona na kujua ya kwamba Yeye alikuwa amesimama katika Uwepo wa Yesu Kristo. Nafikiri lingekuwa ndilo jambo la kushangaza sana ambalo—ambalo mtu ye yote, mwamini ye yote, angeweza kuwazia; kujua, na kujua dhahiri, ya kwamba anasimama moja kwa moja katika Uwepo wa—wa Bwana Yesu Kristo, Hakim wake wa kutisha, Mkombozi wake, Naye atakuwa Hakim wake kwenye ile Hukumu.

²¹ Sasa swali hili lililoulizwa. Wayunani hawa walikuwa wamekuja kwenye ibada, na labda walikuwa waongofu wa dini ya Kiyahudi. Nao walikuwa wamekwenda kule kwenye sikukuu, kwa hiyo hapana shaka walikuwa waongofu. Nao walikuwa wamesikia habari za Yesu. “Imani chanzo chake ni kusikia, na kulisikia Neno la Mungu.”

²² Sasa, mahali fulani katika Maandiko, hapana shaka walikuwa wamesikia ama kusoma Masihi angekuwa ni Mtu wa namna gani. Kwa hiyo wakijua kama wao wangeweza . . . Mtu huyu anayedai kuwa Masihi, ilibidi awe na sifa ambazo Masihi angekuwa nazo.

²³ Sasa, kulikuweko na wengi, kulikuweko na masihi wengi wa uongo waliozuka, tunajua hata kulikuweko na mmoja aliyeitwa Yesu aliyeinuka kabla tu ya yule Mtiwa Mafuta. Masihi alikuwa mtiwa mafuta, ambalo maana yake ni “Kristo, ninii. . . M—Mtu aliyetiwa mafuta na Roho Mtakatifu, utimilifu wote wa Mungu, alikuwa Masihi, Mungu katika Mwanadamu. Mwanadamu na Mungu wakawa mmoja, hapo Mungu alipoingia katika Mwanadamu.

²⁴ Sasa, Wayunani hawa walikuwa wadadisi sana. Walikuwa wamesikia baadhi ya mambo makuu juu ya Jamaa huyu Ambaye alitoa madai haya, nami ninawapenda kwa ajili ya kuwa waaminifu vya kutosha kuchunguza jambo hilo. Nafikiri, kama sote tungefanya mambo mengi zaidi ya namna hiyo, tungeangalia mambo tunayosikia habari zake, na kuyapima kulingana na Neno.

²⁵ Sasa, Mungu habadilishi kamwe njia Yake ya kufanya mambo. Yeye daima hudumu vile vile. Sasa, Yeye hawezi kubadilika, kwa maana uamuzi wa kwanza wa Mungu ni Wake; yeye daima hana budi kudumu na uamuzi huo, wakati anapoitwa jukwaani, kama leo hii.

²⁶ Mungu alienda kutazama tukio wakati dhambi ilipotendwa hapo awali katika bustani ya Edeni, Naye ilimbidi kufanya uamuzi jinsi atakavyomkomboa mwanadamu. Naye alitoa uamuzi Wake kwa kumkomboa kwa Damu iliyomwagika ya Mtu asiye na hatia, na Yeye hajabadilisha jambo hilo. Tumejaribu kuwaelimisha, tumejenga minara na miji, na theolojia na elimu mbalimbali, na—na madhehebu ya kanisa, na kuwaingiza kwenye madhehebu; na jambo hilo kamwe halijafaa kitu, na kamwe halitaa kitu. Mungu humwokoza mwanadamu kwa Damu iliyomwagika ya Asiye na hatia. Yeye kamwe habadilishi jambo hilo, haidhuru tunafikiria njia iliyoa nzuri jinsi gani. Ni, huo ni uamuzi wa Mungu.

²⁷ Na hawezi kufanya uamuzi, jambo moja leo, na jambo lingine kesho. Wakati anapofanya uamuzi mmoja, Yeye ni mkamilifu. Yeye kamwe haghairi jambo hilo. Mungu anaposema jambo lo lote, ni la kweli Milele, kwa maana Yeye ni wa Milele na Maneno Yake ni ya Milele.

²⁸ Mungu, akijua mwisho kutoka mwanzo, kwa hiyo aligawa kwa ninii Wake—ulimwengu Wake sehemu fulani ya Neno kwa ajili ya kila kizazi kinachokuja. Yeye alituma manabii katika Agano la Kale, tunafundishwa jambo hilo katika Waebrania 1, “Mungu, katika nyakati nyingi na kwa njia nyingi alisema na baba zetu, katika manabii; katika siku hii ya mwisho kwa Mawanawe, Kristo Yesu.” Sasa laiti tungalichunguza Andiko hilo vizuri sana!

²⁹ Wakati Yesu alipokuwa duniani Naye akasema Yeye ni Mwana wa Mungu, wao walimhukumu. Alisema, “Mbona

mnanihukumu Mimi ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu, wakati mnapowaita wale Ambao walijiliwa na Neno, 'miungu'? Ibrahimu alihesabiwa kuwa mungu, Eliya alikuwa mungu, Isaya alikuwa mungu, kwa maana Neno la Mungu liliwajilia. Nao walikuwa, kwa sehemu, miungu. Yesu alisema walikuwa miungu. Yeye alisema, "Mnawaita 'miungu.'"

³⁰ Sasa, mnaona, wakati mtu huyo amelipotiwa mafuta, kama vile Yusufu, alimdhahirisha Kristo; wakati Musa alipotiwa mafuta, alionyesha mfano wa Kristo; wakati Daudi alipotiwa mafuta, alimdhahirisha Kristo. Wote wakielekeza kwa Kristo, Naye alikuwa utimilifu wa Neno. Neno lilidhihirishwa ndani Yake. Yeye alikuwa Mtiwa Mafuta aliyekamilifu. Wao walikuwa na Nayo kwa sehemu; sisi tunayo kwa sehemu. Yeye alikuwa yule Mtiwa Mafuta. Mpango wote wa Mungu ulikuwa ndani Yake. Mpango wa Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuukomboza ulimwengu uliopotea, ulikuwa ndani Yake. Yeye alikuwa Neno, na Yeye angali ni Neno, "yeye yule jana, leo, na hata milele." Kumbuka, Yeye aliwajilia wale mababa, katika manabii, akajijulisha Mwenyewe kupitia kwa manabii; na halafu katika siku hii ya mwisho, katika Mwanawe, Kristo Yesu. Alikuwa Mungu aliyedhihirishwa.

³¹ Angalia, Neno daima humjia nabii. Mungu kamwe hajafanya kazi kamwe kupitia kundi fulani la watu. Yeye hutenda kazi kupitia kwa mtu binafsi. Alifanya kazi katika siku za Nuhu, kupitia Nuhu. Alifanya kazi katika siku za Musa, kupitia Musa. Alifanya kazi katika siku za Eliya, kupitia Eliya, kupitia Elish-...-liya, kupitia Isaya na hao manabii, walipokuwa wakitokea katika zile nyakati.

³² Harafu wakati Yeye alipokuwa hapa, Yeye alidhihirishwa kikamilifu; si katika Mafarisayo, Masadukayo, lakini katika Yesu Kristo. Yeye alikuwa ni Neno. Hiyo ndiyo sababu aliweza kusema yale aliyosema. Hayo ndiyo matamshi ambayo Yeye angeweza kufanya. Sasa, hawa Wayunani walijua jambo hili, mnanona.

³³ Kupitia katika kila wakati, Mungu alipanga kiasi fulani cha Neno, nayo makanisa wanavurugikiwa na jambo hilo kabisa, halafu Yeye anamtuma nabii miongoni mwao na kulithibitisha Neno hilo. Ni kama tu wakati mwingine wote, tunazungumza leo na kusema Wamethodisti...

³⁴ Waluteri walisema, "Mtu unapoaamini, hayo ndiyo tu yanayokupasa kufanya; unanehesabiwa haki kwa imani, kuamini." Wengi walisema waliaamini, wala hawakumpata. Tunajua jambo hilo.

³⁵ Moja kwa moja akaja Wesley pamoja na kile kinachoitwa, "kazi ya pili ya neema," kutakaswa, "Wote ambao wanapiga makelele, na wametakaswa, wamempata." Wengi walipiga makelele, wala hawakumpata."

36 Ndipo wakaja Wapentekoste, wakasema, “Wote wanaonena kwa lugha, wanaye.” Wengi walinena kwa lugha, na hawakumpata.

37 Ndipo wakaja Wanasayansi Wakristo, na wakasema, “Ni upendo, tunda la Roho.” Wengi wao wanaonyesha tunda la Roho, wala hawajampata.

38 Hao Mafarisayo wangeweza kuonyesha tunda la roho mara kumi ya vile angaliweza kuonyesha. Uliwahi kujua hilo? Vipi kama ningalichukua, tuseme. . . Na Mungu na anisamehe, lakini nitachukua upande ule mwingine, nitasema, “Kuna Jamaa fulani hapa Dallas, Jamaa mdogo tu aliyekulia hapa chini, po pote pale, kwenye. . . mtaa mchafu hapa chini, anayejiita Mwenyewe Nabii, kule chini Galilaya. Huyu hapa, akizunguka huku na huku. Nimewakusanya ninyi watu pamoja kuwaonyesha kuna shida gani. Mtu huyu anadai kuwa ni Nabii.”

39 “Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani. Ni nani aliyesoma tangu utotoni hadi utu uzima, ila maskini kuhani wako mcha Mungu? Ni nani aliyeshikamana na baba yako na mama yako, ulipozaliwa, ila maskini kuhani wako mcha Mungu? Ni nani kuchukua kwenye mikono yao, akakutahiri na kukuweka wakfu kwa Bwana, siku ya nane, ila ni maskini kuhani wako mcha Mungu, ni nani ajaye kwako uwapo u mgonjwa na mhitaji, ila maskini kuhani wako mcha Mungu? Ni nani aliyesoma na kutoa dhabihu, maishani mwao mwote ujanani, kujifunza torati zote na kadhalika, ila maskini kuhani wako mcha Mungu? Je! Jamaa huyu mdogo alitoka wapi, huyu Yesu wa Nazareti? Alitokea shule gani? Yeye ni wa madhehebu gani? Ana kadi gani ya ushirika? Hana. Sasa jambo pekee analofanya ni kuwahukumumu hao walio nayo. Jamaa huyu ni nani hata hivyo?”

40 “Na nyinyiwafanyi biashara! Yehova alihitaji mwana-kondoo kwa ajili ya sadaka, damu. Na maskini kasisi wenu mcha Mungu akatengeneza mazizi pale. Ninyi watu ni wafanya biashara, nanyi mnauza hariri na kadhalika, naye aliwatengenezea mahali pale nje ili ninyi wafanyi biashara mngeweza kununua kwa fedha zenu, mwana-kondoo, mpate kumtoa kwa ajili ya dhambi zenu. Jamaa huyu kijana mdogo amefanya nini? Alikuwa kule na kupiga mateke vitu hivyo na kuvipindua; akawatazama kwa hasira, akawapiga na kuwafukuzia nje, akapindua meza za wenye kuvunja fedha. Ungeweza kuita jambo hilo tunda la Roho? La, huwezi, hata anajaribu kuwafanya msiokolewe; damu yenu, ile damu ambayo Yehova alihitaji. Hilo halingeweza kuwa ni la Yehova!” Unaona jinsi lingesikika ni jambo la uongo?

41 Je! hao makuhani siku hiyo, ama hao manabii, wakati Yohoshafati na Ahabu walipoketi pamoja, na makuhani mia nne waliofunzwa vizuri, kutoka shuleni, walipokwea kule na kumwambia Ahabu na hao wengine, “Hiyo nchi ni yenu. Si

halali ya kwamba Wa—Wafilisti wajaze matumbo yao kwa ngano ambayo ni mali ya Israeli. Mwenyezi Mungu alitupa hii sisi. Na BWANA ASEMA HIVI, kwea!”

⁴² Lakini mwajua, Yehoshafati alikuwa mtu wa kiroho, hilo halikusikika sawa. Akasema, “Je! huna mmoja zaidi unayeweza kumtaka ushauri?”

⁴³ Kasema, “Nina mmoja, lakini namchukia.” Naam. Hakika. Kasema, “Yeye daima anatabiri maovu. Anawahukumu watu wetu, katika kila jambo analofanya. Yeye hatakubaliana na hao wengine.”

Kasema, “La! mfalme asiseme hivi, bali mlete.”

⁴⁴ Na wakati maskini Mikaya mwana wa Imla alipokuja, aliona ono. Akalinganisha ono lake na Neno. Na hapo alipoona ono lake vimelingana na Neno, akasema, “Kwea, lakini niliwaona Israeli wakitawanyika kama kondoo asiye na mchungaji.” Unaona nani aliyekuwa ndiye wa kweli? Wao kweli walikuwa na kitu, na hiyo nchi kweli ilikuwa yao, lakini ilikuwa ni yao chini ya masharti.

⁴⁵ Na vivyo hivyo na Baraka nazo, za siku hii ya mwisho, ni za kanisa hili, lakini ziko chini ya masharti. Huna budi kutimiza masharti hayo. Kama huwatimiza, unaweza kuwa na kila namna ya ibada za uponyaji, ibada za kupiga makelele, ibada za kusifu, ibada za tunda, ibada za kunena kwa lugha, na hazitakufaa kitu hata kidogo. Huna budi kuja kwa sharti la Mungu.

⁴⁶ Hiyo ndiyo sababu Wayunani hawa walitamani kumwona Mtu huyu. Walijua katika Neno ya kwamba huyu Masihi alipaswa kuwa, nao walitaka kumwona. Walikuwa Mataifa. Walikuwa ni wamesikia habari Zake, nao walitaka kumwona.

⁴⁷ Sasa, kama walitaka kumwona Yeye nao walipewa nafasi hiyo, je! hudhani ya kwamba hapa Dallas, usiku wa leo, kama Yeye alisema katika Maandiko, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” nasi tunataka kumwona Yeye, je! hudhani ya kwamba Yeye angetupa jambo lile lile? Kumbuka, kama hafanyi hivyo, Yeye si yeye yule jana, leo, na hata milele. Mimi ninaamini ni yeye yule. Mungu katika siku hii ya mwisho ametendea watu mambo ya ajabu!

⁴⁸ Inanikumbusha kabisa habari za mwanamke mmoja, hapa si muda mrefu uliopita, huko Louisville, Kentucky. Alikuwa na mvulana mdogo kama, loo, umri wa miaka miwili ama mitatu. Na maskini mtoto huyo alikuwa na... hapana shaka aliisha anza kupatwa na—na matatizo ya ubongo. Naye alikuwa amempeleka kwa daktari, naye daktari alikuwa amemtibu kwa muda fulani. Naye alionekana anazidi kuwa mbaya zaidi, kulingana na mamaye. Lakini kwa upande wa daktari, yeye alisema, “Ninaamini ana nafuu.”

⁴⁹ Kwa hiyo mama yake akampa jaribio la ishara fulani. Akampeleka kwenye soko kuu la hela kumi, naye akachukua

kitu fulani kidogo ambacho kingemvutia mvulana huyu mdogo, naye—naye hata hakukiangalia. Basi akaenda kwenye kaunta nyingine, akachukua kitu fulani kilichopaswa kumvutia, bastola ndogo ya kuchezea ama cho chote kile, na—na bado haingemvutia. Naye akafanya kila kitu ambacho alijua, na watu wakaanza kumwangalia mwanamke huyo akianza kupandwa na wenda wazimu. Ndipo akaenda mahali palipokuwa na—na kengele ndogo, naye akaitwaa hiyo na kuitingisha, kama wazimu, mbele ya macho yake, na kusema, “Mpenzi, angalia!” Na maskini mtoto huyo alikodoa tu macho angani. Ndipo huyo mama akaangusha kitu hicho kidogo sakafuni, akaanza kulia kwa sauti kuu. “Mama wee! Hapana,” akalia kwa sauti kuu.

⁵⁰ Ndipo baadhi ya watu sokoni wakaenda kumsaidia, na kuona kuna shida gani. Akasema, “Mvulana wangu mdogo, daktari anasema ana nafuu, lakini hana nafuu. Kitu cho chote kinachopaswa kumvutia, mvulana mdogo kama huyo, hakimvutii. Yeye anakodoa tu macho angani.”

⁵¹ Nafikiri hiyo ndiyo hali imelipata kanisa letu. Mungu ametikisa kila kipawa ambacho alioahidi katika Biblia, mbele yetu, na tungali tunakodoa macho angani, kana kwamba wanatazamia jambo lingine. Yanaonekana kuwa ni hali ya kiroho ya kanisa, kwamba wanashindwa kuona saa ambayo wanaishi. Wanatafuta miasho ama kitu fulani, kitu fulani mbali huko katika siku zijazo. Binadamu daima anafanya hivyo; daima yeye anambariki Mungu kwa yale aliyofanya, akitazamia yale Yeye atakayofanya, huku akipuuzia yale anayofanya sasa hivi. Mnashindwa kuona saa tunayoishi!

⁵² Hilo ndilo hao Wayunani walilotaka kujua, kwamba ilikuwa ni wakati gani na huyo Masihi ni Mtu wa jinsi gani. Ile sehemu ya Maandiko iliyofunuliwa kwa siku ile, kama huyo Masihi alitimiza hilo, hilo ndilo thibitisho! Lile Neno lililothibitishwa la wakati huo ndilo ushuhuda; si kwamba ilimbidi awe na matunda ya Roho, ilimbidi kuwa mwa—mwana sheria kwenye mahakama ya—ya haki, kwa ninii Yake, ama moja ya madhehebu ya Mafarisayo ama Masadukayo. Yeye alikuwa dhihirisho la Neno la Mungu ambalo liliahidiwa la saa hiyo.

⁵³ Je! mnataka kuona tunda la Roho ni nini? Angalia kile Biblia inachoahidi kwa ajili ya wakati fulani, halafu angalia jambo hilo likithibitishwa. Huo ndio ushuhuda. Yesu alisema, “Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnafikiri mna Uzima wa Milele, Hayo Ndiyo yanayonishudia Mimi. Hayo ndiyo yanayothibitisha Mimi ni Nani.”

⁵⁴ Tunaangalia sasa, Andiko moja kabla hatujaingilia jambo lingine. Yesu alisema, wakati alipokuwa hapa duniani, katika Kitabu cha Luka, ya kwamba, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu,” sasa angalia, “na kama ilivyokuwa katika siku za

Nuhu, kabla ya ile gharika.” Sasa Yesu alikuwa akisoma Biblia ile ile ambayo mimi na wewe tunasoma. Na mambo hayo yote yalikuwa ni vivuli. Sasa kama ukitaka kujua ilivyokuwa kabla ya siku ya Nuhu, rudi nyuma na usome Mwanzo. Yeye alisema tu, “Walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa.”

⁵⁵ Lakini kama ukiangalia, rudi nyuma na usome Mwanzo 6 na uone humo kile kilichotukia, tunaona humo huko nyuma, ya kwamba, “Wakati wana wa Mungu walipowaona binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri, walijitwalia wanawake,” mahakama ya talaka. Wana wa Mungu! “Watu wenye sifa,” watu mashuhuri.

⁵⁶ Angalia leo, ma—maafisa wetu, watu mashuhuri wa ulimwengu, kama huyu kabaila mkubwa kule Uingereza hivi karibuni tu, gazeti la *Life* liliandika makala yake, aliyekutwa na wanawake hawa wavua nguo, na kadhalika. Mwangalie gavana wetu wa New York, na nchi zingine zote jirani, huo uzinzi. Angalia talaka. Marekani inayaongoza mataifa katika talaka, wengine wote ulimwenguni. Tazama wanawake, vile wanavyovoa na kutembea mitaani; na jinsi ambavyo wanaume, karibu jambo la kwanza kabisa linalowaziwa, leo, ni jambo la kizinzi. Kila burudani, kwenye sigara, wiski, cho chote kile, ama mchezo fulani mwingine, ama ninii fulani. . . haina budi iwe na mwanamke fulani mzinzi ndani yake. “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu!”

⁵⁷ Yesu alisema, “Na kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma!” Kumbuka, Yeye hakulizungumzia jambo hilo. Hebu na tuchore picha ya Sodoma. Kulikuweko na tabaka tatu za watu ulimwenguni, daima; nao ni waamini, wanaojifanya waaamini, na wasioamini. Wamo katika kila kundi. Tutazungumzia jambo hilo labda usiku mmoja, katika juma. Lakini katika wakati huo, kulikuweko na wasioamini, Wasodoma; kulikuwako na wanaojifanya wanaamini, ambao walikuwa ni Lutu na kundi lake; na kulikuwa na walioitwa na walioteuliwa, ambao walikuwa ni Ibrahimu, ambao hawakuwa kule Sodoma.

⁵⁸ Malaika watatu walishuka kabla tu yule mwana aliyeahidiwa hajaja. Kwamba, Ibrahimu alikuwa mgeni, naye alikuwa amemtazamia mwana aliyeahidiwa; naye Lutu alikuwa amesahau ahadi yote, na akatoka akaingia Sodoma; na Wasodoma hawakumwamini, kwanza. Lakini sasa angalia, asubuhi moja yenye joto, Wenye Uhai watatu walishuka kutoka Mbinguni. Nao walipomjia Ibrahimu, Mmoja wao alibaki pamoja naye. Na wawili wao wakashuka wakaenda Sodoma, kuwaita waliosalia Sodoma, Lutu na hao walioambatana naye, Naye alipata tu watatu; wanane katika siku za Nuhu.

⁵⁹ Sasa hilo ni tamshi zito kweli kwa siku hii inayokuja, “kama ilivyokuwa,” watatu na wanane.

Angalia, kulikuwako na Mmoja, hata hivyo, aliyemjia Ibrahimu.

⁶⁰ Sasa yule aliyeshuka akaenda Sodoma, yeye...wao walihubiri chini kule, wale wawili ambao waliingia kule, walihubiri na kuwaambia ya kwamba wakati ulikuwa umekaribia, ulimwengu wa Mataifa ulikuwa unaenda kuchomwa moto. Sasa angalia picha ya Sodoma ya siku hii; si Nuhu, yale maji; lakini wakati huu moto, kuuangamiza ulimwengu wa Mataifa.

⁶¹ Nao waamini wa kweli wa Kimataifa wanamtazamia Mwana aliyeahidiwa, Mwana wa Mungu, nasi tumengojea. Wao hawako Sodoma. Wameitwa watoke.

⁶² Sodoma ilikuwa ni yule mfuasi vuguvugu wa kanisa. Na pale alikuwepo mtu kama Billy Graham wa kisasa aliyeshuka akaenda Sodoma, miongoni mwa madhehebu, Oral Roberts fulani. Nao wako kule wakitwaga, kwa Injili, ambayo iliwatia upofu. Angalia ishara ambayo aliitenda kule, wao.

⁶³ Sasa mwangalie Ibrahimu, yule mteule, katika kundi lake, Mmoja alibaki kule nyuma na akawafanyia ishara.

⁶⁴ Unajua, katika historia yote ya ulimwengu, historia yote ya kanisa, hapajakuwa kamwe na wakati hata mmoja, ambapo mtengenezaji ye yote, ama mtu ye yote, aliyewahi kuwa na huduma kuu kwa Mataifa, ambaye jina lao limepata kuishia na h-a-m, kama vile I-b-r-a-h-i-m-u, mpaka sasa. Huyu ni G-r-a-h-a-m, herufi sita. Ibrahimu ni herufi saba. Herufi sita, G-r-a-h-a-m. Billy Graham, mwanaufufuo mashuhuri ambaye yuko chini kule Sodoma, miongoni mwa makanisa hayo ya kimadhehebu, akiita awezao kuita. Tume kuwa na akina Billy Sunday, Finney, Sankey, Moody, Knox, Calvin, na kadhalika, lakini kamwe si akina G-r-a-h-a-m ama lo lote linaloishia na h-a-m, kamwe hatujawahi. Kuna mmoja chini kule kwa kanisa la kawaida, huko Sodoma, anayeishia na h-a-m, linalomaanisha, "baba wa mataifa."

⁶⁵ Halafu kulikuwa na Mmoja aliyebakia juu kule na Ibrahimu, aliye keti na hema yake, mgongo umeelekea kwenye hema, Naye akasema, "Ibrahimu," si Abramu, ambavyo aliitwa siku chache kabla ya hapo. "Ibrahimu, yuko wapi mke wako, Sara?" S-a-...r-a, si S-a-r-a-i, unaona. "Yuko wapi mkeo, Sara?"

Akasema, "Yuko huko kwenye hema, nyuma Yako."

⁶⁶ Akasema, "Nikutarudia. Nita-," Mimi, kijina cha kumtaja mtu, "nitakuzuru kulingana na ahadi niliyokupa."

⁶⁷ Naye Sara, akiwa na umri wa miaka mia moja, hemani, akacheka kimoyomoyo, akisema moyoni mwake, "Ninawezaje, niwapo mkongwe, kupata furaha tena na bwana wangu, naye ni mzee, Ibrahimu, kama vijana, ama watu wa maisha ya jinsia yaliyoisha miaka mingi iliyopita?" Yeye alikuwa na umri wa

miaka tisini, na Ibrahimu alikuwa na miaka mia moja. Kasema, “Kupata tu raha na bwana wangu, yeye akiwa mzee, pia?”

⁶⁸ Naye yule Malaika, yule mjumbe aliyetumwa kwa kanisa la kiroho, alitambua alichokuwa nacho, yale aliyosema moyoni mwake. Naye akasema, “Kwa nini Sara alitilia shaka jambo hili, unaona, akisema moyoni mwake, ‘Mambo haya hayawezekani?’”

⁶⁹ Na Sara akajaribu kukana hilo. Lakini kwa kuwa alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu. . . Kutokuamini kwake kungalimhukumu, lakini Mungu hangeweza kumwua, maana alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu. Kanisa lingalihukumiwa muda mrefu uliopita, lakini ni sehemu ya Kristo.

⁷⁰ Angalia ile ishara aliyofanya, akimwambia yale aliyokuwa akifanya, huku amempa kisogo. Yesu alisema jambo hilo lingejirudia, “katika siku za kuja kwake Mwana wa Adamu.” Tunamwona Billy Graham, tunauona moto ukiwa tayari kushuka kanisa likitazamia Mwana wa ahadi. Haya basi, kila kitu kiko sawasawa kwenye mstari kabisa, kikingojea saa hiyo, yule Mwana wa ahadi.

⁷¹ Basi kumbuka ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu aliona. Nasi ambao tumezaliwa kwa Roho wa Kristo, ni Uzao wa kifalme wa Ibrahimu. Yesu aliahidi ya kwamba uzao wa kifalme wa Ibrahimu ungeona ishara ile ile ambayo baba yao Ibrahimu aliona, kabla ya kuja kwa yule Mwana wa ahadi. Hapakuwa na ishara nyingine zaidi. Ibrahimu; mara moja Sara akawa mja mzito, na Isaka akawasili. Ishara ya mwisho ilikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili wa mtu.

⁷² Sasa mtu fulani aliniambia, kasema, “Ndugu Branham, huamini ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu!”

⁷³ Vema, Ibrahimu alisema alikuwa hivyo. Alimwita, “Elohimu.” Na tazama uone kama halijaandikwa kwa herufi kubwa ya L. Angalia kama katika mwanzo wa asili, haliko vile vile lilivyokuwa, “Hapo mwanzo, Mungu aliumba. . .” *Elohimu*, “Yeye ajitoshelezaye kwa yote.”

⁷⁴ Mungu akijidhihirisha Mwenyewe katika Kanisa Lake, miongoni mwa watu Wake. Yesu alisema. . . Hapa alikuweko Mungu amedhihirishwa katika Mwanadamu, Yesu Kristo, “yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kanisa limepitia katika kila aina ya ishara. Vema, halafu wakati Mungu anapotikisa ile ishara ya mwisho mbele zao, wao wanakodoa macho angani. Mungu na aturehemu! Tuna wakati gani wa neema? Huenda muda umeenda zaidi sana kuliko tunavyowazia. Kumbukeni nukuu yangu ya kwanza; watu wataendelea moja kwa moja wakifikiri wanaokolewa, kama Sodoma.

⁷⁵ Yeye alikuwa nini? Hao Wayunani waliona kitu gani ndani Yake? Yeye alikuwa nini? Cho chote walichoona ndani Yake wakati huo, cho chote walichotafuta, hapana shaka walikiona.

⁷⁶ Sasa angalia katika Kumbukumbu la Torati sura ya 18, aya ya 15 hadi 20, Musa. Mungu alimwambia Musa jambo hilo. Naye Musa aliwaambia watu. “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii aliye kama mimi. Itakuwa, yule ambaye hatamsikia, atakatiliwa mbali na watu wake.” Mungu kamwe habadilishi kamwe mpango Wake.

⁷⁷ Sasa Wayunani walikuwa wakitazamia Nabii. Sasa, hawajapata kuwa na nabii kwa miaka mia nne, tangu Malaki. Lakini hao Wayunani walijua kwamba Neno hilo la ahadi kwa siku hiyo lazima liwe Nabii, “Bwana Mungu wako atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.”

⁷⁸ Maana, Neno humjia nabii tu, si kwa kitu kingine bali kwa... Ni wangapi wanaofahamu jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Angalia, ni kamilifu sana hivi kwamba wakati Yohana alipokuwa ndiye nabii aliyekuwa amesimama majini, akibatiza, na Yesu akaja Kwake majini, Neno lilikamjia nabii. Yeye alikuwa Neno, Naye akamjia Yohana majini. Mungu kamwe habadilishi utaratibu Wake, Yeye kamwe habadilishi njia Yake. Yeye ni Mungu asiyebadilika. Sasa, makanisa hayakuamini jambo hilo, hata kidogo, lakini jambo hilo halikubadilisha mpango wa Mungu. Uliendelea moja kwa moja.

⁷⁹ Sasa, Petro, baba yake alikuwa Mfarisayo. Hapana shaka, Andrea, akiwa ni mfuasi wa Yohana, alimsikia akitambulishwa.

⁸⁰ Kasema, “Yule pale Masihi, ninaona Nuru juu Yake, kama hua ikija juu Yake,” akashuhudia. Kasema, “Yeye aliyeniambia huko nyikani, ‘Nenda ukabatize kwa maji,’ alisema, ‘Yeye Ambaye utamwona Roho, ile Nuru, kama hua ikishuka.’” Ilikuwa labda ni Nguzo ile ile ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli jangwani, ikishuka juu Yake, sababu hiyo ilikuwa ni yule Aliyetiwa Mafuta, yule Logos. Ikashuka juu Yake, na yeye akasema, “Ninashuhudia, huyu ni Masihi!

⁸¹ Kwa hiyo Petro akaja pamoja na Andrea, kwenye mkutano.

⁸² Hebu na tuone Yeye alikuwa nini. Na kama tukiona alikuwa nini, basi tutajua Yeye ni nini sasa. Na jinsi walivyolitambua jambo hilo wakati huo, inapaswa kuwa ndiyo njia ile ile ya kulitambua leo hii, kwa maana ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa tukiwa na msingi huu wa ahadi Yake, hivi ndivyo Yeye angefanya. Angalia.

⁸³ Sasa tunaona, ya kwamba Petro alipokuja kwenye kusanyiko, mahali pale ambapo Yesu alikuwa; Yesu, ingawa hakuwa amemwona hapo awali, aligeuka akamwangalia, na kusema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.” Si kwamba tu alimjua, lakini alimjua baba yake mzee mcha Mungu ambaye alimfundisha. Naye Petro, bila elimu ya kutosha kutia sahihi jina lake, alihesabiwa kuwa ni mtu mjinga na asiye na maarifa, ambaye ilimpendeza Mungu kumfanya askofu

huko Yerusalemu, naye Yesu akampa ufunguo wa Ufalme na kumfanya kichwa cha kanisa. Mtu huyu, juu ya ufunuo huu uliofunuliwa, akijua kile Masihi alichopaswa kuwa, alisema, alimtambua Yeye kama Masihi, na kumsujudu, kwa maana Yeye alifanya jambo hilo.

⁸⁴ Kulikuweco na mmoja aliyesimama pale, jina lake Filipo. Haikubidi afanyiwe hivyo. Lakini alikuwa na mwalimu wa Biblia aliyemjua vizuri sana, jina lake Nathanaeli. Kama utapaangalia mahali Yesu alipokuwa wakati huo, ilikuwa maili kumi na tano kuuzunguka mlima huo, kama siku mbili. Naye Filipo anatoka anaenda na anampata Nathanaeli chini ya mti, akiomba, naye akamleta. Hapana shaka, kama tungaliweza kuingilia mazungumzo yao, wakati wakienda, wanasema, “Angalia, njoo, uone ni Nani tuliyempata; Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.”

⁸⁵ Akasema, “Sasa, laweza neno jema kutoka Nazareti?”

⁸⁶ “Angalia, unakumbuka, tumesoma katika Maandiko, Masihi atakuwa nabii.”

⁸⁷ “Loo, hakika, Biblia ilisema hivyo, Musa. Sisi ni wanafunzi wake. Yeye alisema Bwana atawaondokeshea Nabii kama alivyo yeye.”

⁸⁸ “Vema, sasa, Yesu wa Nazareti ndiye Nabii huyo. Unamkumbuka yule maskini mvuvi, Simoni, anayeishi karibu na pale?” “Naam.” “Yeye ni—yeye alikuwa mwana wa Yona.” “Naam.” “Ulinunua samaki kutoka kwake wakati mmoja, naye hata hangeweza kutia sahihi risiti.” Naam.”

⁸⁹ “Alikuwa karibu Naye, basi akasema, ‘Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona.’ Haingenishangaza mimi kama hatajua yote kukuhusu wewe ukija.”

⁹⁰ A-ha, ilimbidi Nathanaeli kuona jambo hili, kwa hiyo akaja pamoja na Filipo. Sidhani aliingia kwenye mstari wa maombi. Huenda aliketi kwenye kusanyiko, ama alisimama kusanyikoni, cho chote kile. Yesu alikuwa akiwaombea wagonjwa.

⁹¹ Na mara Yesu alipomwangalia, Alisema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.” Sasa, Yeye hakumjua kwa jinsi alivyovaa. Wakazi wote wa Mashariki huvaa namna moja, wana vilemba na ndara, na—na majoho yanayopwaya, alikuwa na ndevu. Akasema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.” Sasa, angeweza kuwa ni Mwislamu, angeweza kuwa... angeweza kuwa Mturuki, angeweza kuwa cho chote kile, lakini Yeye alijua alikuwa Mwisraeli na hakuwa na hila ndani yake? Na jambo hilo lilimnyenyekeza kabisa.

Ndipo akasema, “Rabi, ulipataje kunitambua?”

⁹² Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwapo chini ya mti, nilikuona.” Hilo lilimaliza. Hilo lilitosha.

⁹³ Hiyo hapo. Huyu hapo Masihi. Akasema, “Wewe ndiye Kristo, Mfalme wa Israeli.” Labda mchungaji wake alikuwa amesimama pale, lakini halikumbabaisha.

⁹⁴ Kulikuwako na hao waliokuwa wamesimama pale, kasema, Mtu huyu ni Beelzebuli.” Ilibidi wawe na kitu cha kuliambia kusanyiko lao, wajua. Kasema, “Mtu huyu anafanya jambo hilo kwa nguvu za Ibilisi. Yeye ni mpiga ramli ama kitu fulani.”

⁹⁵ Yesu akasema, “Mnaniita Mimi hilo, jina baya; kazi za Mungu, jina baya?” Akasema, “Mkisema hivyo kuhusu Mwana wa Adamu, nitawasamehe. Lakini wakati Roho Mtakatifu atakapokuja,” wakati huu wa sasa, “kufanya jambo lile lile, neno moja dhidi Yake halitasamehewa katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ule ujao.” Hivyo ndivyo alivyosema. Ninaamini anayosema Yeye ni kweli.

⁹⁶ Filipo alitambua, kwa jambo hilo. Kwa nini? Kulikuwako na jambo hilo, baada ya miaka mingi bila nabii, na hapa Mtu huyu alimjua yeye, na alijua shida yake, na yale aliyokuwa anafanya.

⁹⁷ Yesu. Upesi sasa kabla hatujafunga. Siku moja, Yeye alikuwa akishuka kwenda Yeriko, ambao ulikuwa chini ya kilima. Lakini alikuwa hana budi kupitia Samaria, ndipo akaenda kupitia katika mji unaoitwa Sikari.

⁹⁸ Sasa kuna mataifa matatu ya watu. Amini unavyotaka kuamini, lakini yapo. Hayo ni watu wa Hamu, Shemu, na wa Yafethi. Sasa angalia, wakati Wayahudi, wao walikuwa wakimtaamia Masihi. Na Msamaria alikuwa nusu Myahudi na nusu Mmataifa, walikuwa wakimtaamia Ma–Masihi. Lakini Mmataifa, sisi watu wa Anglo-Saksoni, tulikuwa makafiri, Wafilisti na kadhalika, mnaona.

⁹⁹ Lakini angalieni, Yeye huwajia tu wale wanaomtaamia. Yeye ataponya tu, usiku wa leo, hao wanaomtaamia kuwaponya. Atawaokoa wale tu ambao wanataamia kuokolewa.

¹⁰⁰ Na sasa mwangalie sasa wakati anapowatuma wanafunzi wake kwenda katika mji mdogo wa Sikari, kununua cha–chakula. Walipokuwa wameondoka, kijana mmoja mwanamke mrembo akatokea, naye alikuwa ni mwanamke mwenye sifa mbaya. Tungemwita, leo, labda kahaba. Huenda wazazi wake walimfukuza wakati alipokuwa msichana mdogo, na hivyo ndivyo alivyopata riziki yake, lakini kulikuwa na kitu fulani katika moyo wa maskini mama huyo mdogo. Alikuwa kwenye saa tano, maana asingeweza kuja pamoja na wanawali wengine wote. Kama mtu ye yote ameshawahi, hapa, kwenda huko India na katika nchi za Mashariki, kwa kuwa mila zao hazibadiliki, hawawezi kuchangamana, watu wazuri na wabaya. Kwa hiyo wao. . .

¹⁰¹ Akapanda akaja, Naye Yesu alikuwa ameketi pale. Katika mandhari ndogo kitu kama hiki, mizabibu hukua nyuma ya kisima. Na kisima cha jumuiya ya mji kilikuwapo pale, nao

watu wanatoka wanakuja kuchota maji. Naye akaja kwenye karibu na adhuhuri, kuchota maji. Ambapo, wanawali wanakuja asubuhi na mapema, kuchota maji, nao wanafulia juu kule na mambo kama hayo. Njia yake ya kupata riziki ilikuwa ni njia tofauti. Kwa hiyo akaja karibu adhuhuri, kuchota yake, wakati wanawali hawakuweco, kwa maana angalifukuzwa atoke kisimani.

¹⁰² Na wakati yeye, bila kuwa na habari na mtu aliyekuwa ameketi pale, aliingiza zile kulabu ndogo kwenye mtungi na kuushusha kwa winchi, kisimani, kisha akaanza kuyachota. Akasikia sauti ikisema, “Mama, nipe maji ninywe.” Naye akaangalia kule, na kulikuweco na Mtu aliyeketi pale, ambaye alikuwa Myahudi.

¹⁰³ Hapana budi alionekana mzee kidogo kuliko alivyokuwa hasa, kwa sababu Yeye alikuwa na umri wa miaka thelathini tu, kama thelathini na mitatu, na Biblia ilisema, “Alionekana kama ana umri wa miaka hamsini.” Wajua, Wayahudi walisema, “Wewe ni mtu ambaye hujapata miaka hamsini, Nawe unasema ati ‘umemwona Ibrahimu?’”

Akasema, “Ibrahimu asijakuwepo, MIMI NIKO.” Mnaona?

¹⁰⁴ Kwa hiyo ndevu Zake hazina budi zilikuwa na mvi kidogo, ama cho chote kile, kama alivyoonekana. Na yule mwanamke akamwanguka. Kazi Yake haina budi ilikuwa na matokeo makubwa sana juu ya maisha Yake ya mwili. Na yule mwanamke akasema . . .

Yeye akasema, “Nipe maji ninywe.”

¹⁰⁵ Naye akasema, “Si desturi Kwako Msamari- . . . ama kwenu ninyi Wayahudi kutuuliza sisi wanawake wa Samaria swali kama hilo.”

¹⁰⁶ Yeye akasema, “Lakini kama ungalijua Yeye ni nani anayezungumza nawe, ungaliniomba Mimi maji ya kunywa.”

¹⁰⁷ Sasa yule mwanamke akasema, “Kisima ni kirefu.” Yeye alikuwa anafanya nini? Alikuwa anawasiliana na roho ya mwanamke yule, unaona. Baba . . .

¹⁰⁸ Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:19, “Amin, amini, nawaambia, Mwana hawezi kufanya neno Mwenyewe, ila lile ambalo anamwona Baba analitenda.” Sasa kumbukeni jambo hilo. Andikeni jambo hilo kwenye vitabu vyenu, mnaona. Yesu kamwe hakufanya hata jambo moja mpaka alipoona katika ono afanye nini. Hiyo ni kweli. Si *kusikia*; “kile *ninachooka*.” “Mwana hawezi kufanya neno ila lile ambalo anamwona Baba akilifanya, ndipo Mwana analifanya hilo vile vile.” Yeye alilitenda katika mchezo wa kuigiza. Hakuna mtu awezaye kufanya Neno bila kweli Mungu kumwambia la kufanya. Sasa angalia, Baba labda alimwambia apande aende Samaria.

109 Na ndipo Mwanamke huyu akasema Naye, Naye akasema, akaendeleza mazungumzo ya yule mama, apate kuishika roho yake. Ndipo wakati alipokuwa akinena kuhusu “kuabudia hapa Yerusalemu,” muda si muda, Yeye aliona shida ya huyo mwanamke ilikuwa ni nini. Sote tunajua ilikuwa ni nini. Alikuwa na waume wengi mno. Na kwa hiyo akasema, “Nenda ukamwite mume wako mje hapa.”

Na akasema, “Si—sina mume ye yote.”

110 Yeye akasema, “Umesema kweli, kwa kuwa umekuwa na watano, naye unayeishi naye sasa si wako.”

111 Basi angalia mwanamke huyu, angalia, naye akiwa katika hali hiyo. (Ninachelewa sana, sana?) Yeye akiwa katika hali hiyo, alijua zaidi kuhusu Biblia halisi kuliko kundi kubwa la wahubiri wanavyojua leo. Na mara Yeye anapooni ninii... Huenda aliwazia ya kwamba ilikuwa ni m—mtu tu anayeona hali yake, na—na alitaka tu ku-... alitaka kumchezea ama cho chote kile, ndipo akasema, “Sina mume!”

112 Yeye akasema, “Umesema kweli. Una watano, naye unayeishi naye sasa si mume wako.”

113 Haraka hiyo mbegu iliyochaguliwa tangu zamani iliyokuwa moyoni mwake ikashika moto. Akageuka, akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe u nabii. Hatujakuwa na mmoja kwa muda wa miaka mia nne, wajua. Tunajua.” Loo, Dallas, msikose jambo hili! “Tunajua. Tunamtazamia Masihi, Aitwaye Kristo. Naye atakapokuja, haya ndiyo atakayofanya. Hii itakuwa ndiyo ishara Yake.”

Yesu akasema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

114 Kwa maneno hayo, akashusha mtungi wake, akakimbia kwenda mjini, kasema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo yale niliyofanya. Yamkini huyu kuwa Ndiye Masihi?” Na Biblia ilisema ya kwamba walimwamini Yesu kwa sababu ya yale aliyosema mwanamke huyo.

115 Sasa hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kama Masihi; si kwa sababu ya vile alivyovaa, kwa elimu Yake, kwa kadi Yake ya ushirika, kwa heshima Yake kati ya wanadamu. Mungu alikuwa ndani Yake, akilidhihirisha Neno aliloahidi. Alisema katika Yohana Mt. 5:39, “Chunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnafikiri mna Uzima wa Milele. Hayo Ndiyo yanayonishuhudia, ama, kuwaambieni kwamba Mimi ni Nani.”

116 “Yeye yule jana, leo, na hata milele.” Ndugu yangu, dada yangu, ninyi ni kusanyiko zuri sana, mtu angeweza kuzungumza usiku kucha. Mnaona kile alichokuwa Yesu wakati huo? Yeye alidhihirishwa, huyo alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika Mtu anayelitwa Yesu Kristo, ambaye ni Mwana wa Mungu, akiahidi, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu,” kila tukio jingine lilibakia vile vile, “ndivyo itakavyokuwa atakapokuja

Mwana wa Adamu.” “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Loo, enyi kanisa, msikodoe macho, lakini mwaminini Bwana Yesu Kristo! *Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.* Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, je! ungetaka kumwona? “Mabwana, tu-. . . Ungemtafutaje? Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye atafanya vile vile.

¹¹⁷ Sasa, mtu fulani angeweza kuja hapa akiwa na makovu ya misumari mikononi mwake, damu na moshi, na mafuta yakimtiririka. Hilo halingefua dafu. Mnafiki ye yote anaweza kufanya jambo hilo. Bila shaka.

¹¹⁸ Lakini jambo ni kwamba, ni kule kudhihirishwa kwa Neno hili la ahadi. Yeye alikuwa Nabii wa Mungu aliyetiwa mafuta. Alikuwa hivyo. Alikuwa Mungu-Nabii. Alikuwa yote waliyokuwa wale manabii, yalikuwa ndani Yake, kuongeza yale mengine aliyokuwa Mungu. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake Mwenyewe. Yeye alikuwa ni Mungu, Imanueli, utimilifu wa Mungu uliotambulishwa kwetu, katika Utu wa Mwanawe Yesu Kristo, sifa ya pili ya Mungu.

¹¹⁹ Angalia sasa, Yeye yu hai leo. Si mfu. Yu hai. Alisema, “Kitambo kidogo, na ulimwengu,” *kosmos*, “utaratibu wa ulimwengu utaniona. . .” mnaona; o, n na a “hautaniona kamwe. Hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi,” Mimi tena ni kijina cha kumtaja mtu, “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari, ama mwisho wa ulimwengu wakati Maandiko haya yatakapotimizwa.” Kote kote huko nyuma, imekuwa ni Mungu Ambaye tumemwamini katika wakati wa Luther, Mungu Ambaye alipiga makelele—katika wakati wa Wesley, Mungu aliyenena kwa lugha katika wakati wa Wapentekoste. Yeye anashuka moja kwa moja kabla yule Mwana wa ahadi hajaja, kuyathibitisha Maandiko Yake. Maandiko yote hayana budi kutimizwa. *Mabwana, tunataka kumwona Yesu.*

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹²⁰ Baba wa Mbinguni, tunataka kumwona Yesu. Naomba aje usiku wa leo, Bwana Yesu. Njoo katika Nguvu za kufufuka Kwako. Nimekuwa nikizungumza kwa muda mrefu, lakini neno moja tu ama mawili kutoka Kwako yatamaanisha mengi zaidi ya vile mtu ye yote angeweza kusema, na halafu jalia Kanisa lisilale. Jalia ninii. . . Dhihirisho la mwisho la Mungu, kama Yeye alivyoahidi, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, kabla ya moto kushuka juu ya Mataifa, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Kivuli, negativu na kilicho halisi vinakaribiana sana, mpaka baada ya kitambo kidogo kutakuweko na wakati wa kuungana.

¹²¹ Tunaona mataifa yanaungana, unaoitwa U.M. Makanisa yanaungana, Baraza la Ekumeni linaungana na Vatican.

Makanisa yote yanaungana pamoja, waamini na wasioamini. Wafanyakazi wanaungana katika vyama vya wafanyakazi.

¹²² Bwana, jalia Kanisa liamke liona ni wakati wake wa kuungana, ya kwamba Yesu anaungana na Kanisa Lake, Mume na Mke. Hivi karibuni sherehe itafanyika nao watakuwa Mmoja. Wakati anapotutikisia ishara ya mwisho, ama kutuonyesha ahadi Yake, jalia tumwone Yesu na kumtukiza Yeye, kwa maana ni katika Jina Lake tunaomba. Amina.

¹²³ Sasa nitaninii, labda, nina dakika kumi ili kutoka katika wakati, kama kila mtu ataitika. Sasa ye yote aliye na kadi ya maombi, sitapata nafasi ya kuwafikia wote usiku wa leo. Tutawafikia, baadaye.

¹²⁴ Sasa Billy yuko hapa mahali fulani, nina hakika. Wakati mwingine wao hata hagawi kadi, lakini ninaamini aliniambia ali- . . . Mna kadi za maombi, sivyo? Inueni mikono yenu. Naam, hiyo ni kweli, maombi. . . [Sehemu tupu. Mtu fulani anasema, “L, moja.”—Mh.]

¹²⁵ L, L, vema. Huyu ndiye yule mtu mgonjwa, mgonjwa sana, pale? Vema. L, namba moja, simama hapa. L, namba mbili, uko wapi? Namba mbili, uko wapi namba mbili? Waweza kuinua mkono wako? Vema, njoo hapa. Ni mama.

¹²⁶ Huyu mvulana hushuka anakuja. Hivi ndivyo ilivyo. Yeye anashuka, na mbele ya wasikilizaji, anazichukua kadi hizi na kuzichanganya zote pamoja, na halafu ukitaka anakupa kadi. Mtu ye yote anaweza kupata kadi, na halafu unaitwa kwa namba hiyo. Hiyo ina maana kwamba mvulana huyo hana habari ni ipi itaitwa. Wakati mmoja sisi, wengi wenu hapa huenda mkakumbuka, tulikuwa na mtu aliyekuwa anauza kadi za maombi mikutanoni, na jambo hilo lingemhakikishia mtu huyo angepanda juu jukwaani. Na licha ya hilo, wakati mwingine ninaanza na moja, na wakati mwingine ninaanza na hamsini, wakati mwingine ninaanza na kumi na nne, ishirini, kumi na sita, kisha ninarudi kinyumenyume na kuchomoa machache hapa. Ni wangapi wamekuwa mikutanoni na kuona jambo hilo likitendeka? Mbona, hakika. Mnaona? Hiyo kadi ya maombi haina uhusiano wo wote na jambo hilo. Na wengi wanaponywa huko nje ambao hata hawana kadi ya maombi.

¹²⁷ Namba moja, mbili, tatu. Ni nani aliye na tatu? Kadi ya maombi namba tatu, inua mkono wako. Kule nyuma, yule mama. Njoo hapa, mama. Namba nne. Kama mtu huwezi kuamka sasa, tutakubeba. Namba nne. Kama wengine. . . Ninaona kuna machela hapa na magari ya walemavu vimewekwa hapa. Kama huwezi kuja, tutakubeba. Namba nne. Namba tano, kadi ya maombi namba tano. Namba sita, saba, nane, tisa, kumi. Hebu hao waje sasa, kwa namba tu, wakiweza. Hebu tuone. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa. Hilo limewafikia? Hilo limewafikia. Hebu na tusimamie papo hapo, kwa muda

kidogo tu. Tumechelewa tu kidogo. Sipendi kuwaachilia mtoke baada ya saa tatu na nusu.

¹²⁸ Sasa, ni wangapi huko nje wasio na kadi ya maombi, nawe unataka Yesu akuponye, na unajua ya kwamba anaweza kukuponya? Inua mkono wako. Sijali kama wewe uko huko kwenye roshani, po pote ulipo. Sasa angalia, kama huninii. . .

¹²⁹ Mwanamke yule aliyeligusa vazi. . . Wakati mnapowaweka kwenye mstari. Mwanamke yule aliyegusa vazi Lake, yeye hakuwa na kadi yo yote ya maombi, labda, lakini yeye alisema. . . Sasa sikilizeni kwa makini sasa. Alisema moyoni mwake, “Ninamwamini Mtu yule. Kama nitaweza kugusa vazi Lake, nitakuwa mzima.” Alikuwa na ugonjwa wa kutokwa na damu. Ni wangapi wanakumbuka hadithi hiyo? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Akapenya kwenye umati wa watu, labda akatambaa kati yao, maskini mwanamke amepauka kwa kuugua, naye akaligusa vazi Lake.

¹³⁰ Nalo vazi la Kipalestina linapwaya. Yeye kata kata hangaliweza kuhisi hilo. Singehisi kama ungaligusa mfuko wangu, na koti langu hunibana. Lakini hayo mavazi ya Kipalestina, nao wana vazi la ndani. Naye akagusa vazi Lake.

¹³¹ Ndipo akasimama akasema, “Ni nani aliyenigusa?” Yule mwanamke akatoka na kurudi kwa makutano. Akasema. . .

¹³² “Mbona,” Petro akasema, “Bwana, hilo haleleti. Kila mtu anakugusa.”

¹³³ Akasema, “Lakini ninaona nimekuwa mnyonge. Nguvu, uwezo, ulinitoka.” Ni wangapi wanakumbuka jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹³⁴ Ndipo akaangalia kila mahali katika makutano mpaka akampata. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Naye akasema, “Imani yako imekuokoa.” Hiyo ni kweli? [“Amina.”]

¹³⁵ Sasa angalia, ewe mhudumu, je! Biblia inasema ya kwamba, “Yesu Kristo,” Waebrania 3, “ni Kuhani Mkuu sasa hivi anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu?” [Wahudumu na kusanyiko wanasema, “Amina.”—Mh.] Wangapi wanajua Biblia husema jambo hilo? [“Amina.”] Vema, kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, yeye angetendaje leo? Kama alivyofanya jana. Hakika.

¹³⁶ Sasa, ninyi, mnaona, haingewafaa kitu kunigusa mimi. Ningekuwa kama ndugu yako, mume wako, baba yako, ye yote yule. Hakungekuwa na nguvu yo yote ndani yangu. Lakini kama wewe, imani yako, inaweza kumgusa Yeye, basi mwangalie akigeuka. Jaribu tu. Usijaribu; hilo ni jambo kubwa leo, la kujaribu. Wewe lifanye!

¹³⁷ Sasa iweni na uchaji sana, mwe kimya. Sasa muda kidogo tu utaonyesha. Mambo haya ambayo nilisema, yalisikika ni mazuri;

lakini, unaona, Je! hayo ni kweli ama si kweli? Hilo ndilo jambo linalofuata. Hawa ndio wote. . .

¹³⁸ Ninawasikia Waislamu wakizungumzia, Makalasinga, Wajaini, Wabudha, loo, jamani, Waislamu, lakini wao hawawezi. . . Wanaweza kuzungumza juu ya jambo fulani lililokuwepo, lakini vipi kuhusu wakati huu wa sasa? Mnaona? Kama Yeye si ninii. . .

¹³⁹ Kama Yeye ni Mungu wa historia, Yeye hatufai kitu leo, kama Yeye ni Mungu wa historia tu. Kama si yeye yule jana, leo, na hata milele, basi Biblia ilikosea.

¹⁴⁰ Sasa, kama anaweza kuniweka katika mapenzi Yake matiifu, kama Yeye anaweza kukuingiza katika mapenzi Yake, halafu afanye kazi kati yetu, mnaona, hapo ndipo Uweza wa Mungu unapokuja.

¹⁴¹ Sasa, kama mtu huyo ni mgonjwa, ninataka aketi papo hapo alipo. Na sasa je! wasikilizaji mnaweza kumwona kutoka hapo mlipo? Yeye ameketi papa hapa.

¹⁴² Leteni kiti chake papa hapa kama mnataka. Lakini unaweza kujisikia kuja hapa kwa namna fulani, bwana? Vema, hebu njoo tu papa hapa uketi. Lete hicho kiti papa hapa, Ndugu Grant, ukiweza, ili mtu huyo aweze kuketi hapa kwa muda kidogo tu. Vema, sasa hebu keti tu chini papo hapo, bwana.

¹⁴³ Nimekuwa nikimwona mtu huyo kwa dakika chache, akitaka kufa. Hapana budi ni mgonjwa sana. Sijui. Na kama ningejua na ningeweza kumsaidia, na nisingetenda hilo, basi sistahili kusimama nyuma ya jukwaa hili hapa na kuzunguza na ninyi watu, ninyi Wakristo.

¹⁴⁴ Lakini mtu huyo labda si mzee kama nilivyo mimi. Na hii ni ninii yetu. . . Labda hatufahamiani. Hunijui, nadhani. [Ndugu anasema, “Ndiyo, nakujua.”—Mh.] Unanijua. Lakini sikujui. [“Nilikuwa kwenye ibada moja huko Jonesboro.”] Loo, uliniona huko Jonesboro, kama miaka kumi na mitano iliyopita, nilipokuwa huko katika mkutano. Ndiyo, bwana. [“Hakika nilikuwako.”] Vema, huo ulikuwa wakati mzuri sana kule. Ninaamini huyo alikuwa Ndugu Richard Reed. [“Naam, bwana.”] A-ha.

¹⁴⁵ Sasa kama mtu huyu aketiye hapa anaugua, kama ningaliweza kumponya na nisimponye, ningekuwa mtu wa namna gani? Lakini siwezi kumponya. Lakini sasa kama tungemwona Yesu, na Yesu angekuwa amesimama hapa amevaa suti hii ya nguo aliyonipa Yeye, sasa je! Yesu angesema, “Njoo hapa na nitakuponya”? Sasa uwe mwangalifu, kama unajua Biblia yako, unaona. La, bwana. Tayari amefanya hilo; hangeweza kufanya hilo leo. Kaishafanya tayari, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu,” kwa mapigo Yake tuliokolewa, “kwa mapigo Yake tuliokolewa,” hasa. Vema. Sasa, lakini Yesu angeweza kujitangaza, kumfanya mtu huyu ajue shida yake

ni nini, ama yuna nini, ama jambo ambalo amefanya. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Na jambo hilo lingemjulisha kwamba Kristo alikuwa hapa.

¹⁴⁶ Maana, mimi simjui. Hii hapa mikono yangu imeinuliwa, mimi . . . yeye alisema alikuwa katika mkutano wa Jonesboro. Hiyo ilikuwa ni miaka kumi na mitano iliyopita. Si—sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu, ni juavyo mimi. Huenda angaliketi nyuma, kesho . . . Vema, simjui mtu ye yote hapa.

¹⁴⁷ Naamini ninamjua huyu ni Bw. Way anayeketi papa hapa. Mwingereza anayeketi papa hapa, ninayemjua, ambaye alianguka akafa kanisani mwangu, hivi majuzi, huko Jeffersonville, Indiana; alianguka akafa. Mkewe yuko pale, mahali fulani hapa, ambaye ni nesi. Nilipokuwa nikiongea, mtu huyo alianguka alianguka akafa, pale pale, akafa. Nikashuka nikaenda nikamwekea mikono, huyu hapa amesimama. Unaona? Unaona?

¹⁴⁸ Laiti ningeweza tu kulinyamazisha kusanyiko muda mrefu vya kutosha mpaka Roho Mtakatifu aweze kushuka. Msisisimkwe. Ketini tu kimya, mnaona.

¹⁴⁹ Sasa, bwana, ninataka uangalie huku, kwa muda kidogo. Nimekuwa nikizungumza, nami ni—niko hapa kukusaidia, sasa. Na kama ninaweza kukusaidia, nitafanya kila niwezalo.

¹⁵⁰ Sasa yale niliyosema hapa katika Maandiko, Mungu anawajibika, kwa sababu ninaamini hizi ni siku za mwisho; Mungu anawajibika ku—kultimiza Neno hilo, na hilo ndilo aliloahidi kufanya. Na kama Yeye angeweza kuniambia jambo fulani ulilofanya, ama shida uliyo nayo, ama kitu kilichokuleta hapa, ama cho chote kile, ungejua kama hilo ni kweli ama si kweli. U—u—ungeshuhudia jambo hilo.

¹⁵¹ Lakini sasa kama nikipanda kuja hapa juu na kukuwekea mikono, niseme, “Mungu atukuzwe, umeponywa! Mungu atukuzwe.” Hilo lingekuwa sawa, hilo ni sawa kabisa, kama ukiamini jambo hilo.

¹⁵² Lakini vipi kama Yeye akikwambia jambo ulilofanya, ama sababu fulani, sababu ya wewe kuwa mgonjwa, ama jambo kama hilo? Basi ungejua, kama angeweza kukwambia yale yaliyopita, bila shaka Yeye angejua, yale—yale yatakayokuwa, ingekuwa sawa. Naam.

¹⁵³ Mnaamini jambo hilo, enyi wasikilizaji? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa ninafanya nini kwa mtu huyu? Ninajaribu kuipata roho yake, kama tu vile Bwana wetu alivyofanya pale kwenye kisima, kwa yule mwanamke. Mimi simjui. Sijapata kumwona. Sasa kuna wengi hapa, wagonjwa, wengi wanaomba.

¹⁵⁴ Na sasa, Baba wa Mbinguni, tunachukua kila roho ndani hapa chini . . . mamlaka yetu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu,

ili kwamba Maandiko Yako yapate kutimizwa. Biblia ilisema hiyo ndiyo sababu Yesu aliponya, “Kusudi Maandiko yapate kutimizwa.” Na hiyo ndiyo sababu unaonyesha rehema katika siku hizi za mwisho, “ili Maandiko yapate kutimizwa.” Ndiyo kwanza tuzungumze habari Zake, usiku wa leo. Tujalie, Bwana, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁵⁵ Sasa niangalie, kwa muda kidogo tu, kuona tu kama Bwana atanifunulia shida yako. Na kama atanifunulia, je! utaninii... kama akiniambia shida yako ni nini. Unaonekana kama u mgonjwa sana. Kama angeniambia shida yako, ama cho chote kile, utaamini basi, unajua haina budi kuwa ni Yeye.

¹⁵⁶ Ni wangapi kwenye kusanyiko wataamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁵⁷ Jambo moja, ni kwamba, unaumwa sana, ugonjwa wa mshipa. Huo mshipa ndio unaokufanya mgonjwa. Hiyo ni kweli. Unaona? Unaona? Sasa hilo ni kweli? Inua mkono wako, kama jambo hilo ni kweli.

¹⁵⁸ Huo ndio unaomfanya mgonjwa, unaona, chini. Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁵⁹ Hili hapa jambo lingine. Una doa upande wa kulia wa uso wako. Una wasiwasi kuhusu jambo hilo. Hebu nikwambie jambo lingine. Unaniamini mimi kuwa nabii Wake? [Huyo ndugu anasema, “Ndiyo, ndugu.”—Mh.] Una doa kwenye kiweo chako cha kulia, pia, chini ya nguo zako. Kama jambo hilo ni kweli, inua mkono wako. [“Hiyo ni kweli.”] Unaona? Unaona? Sasa unaamini? [“Naamini.”] Nenda zako ukawe mzima. Yesu Kristo anakuponya. Nenda na uamini jambo hilo. Usitilie shaka, hata kidogo, bwana. Hebu njoo tu hapa, soge hapa, ndugu. Nenda tu, ukiamini, sasa, na kila kitu kitakuwa sawa kwako.

¹⁶⁰ Mnaamini sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Iweni tu na imani. Sawa. Hilo, mwajua, sikujua.

¹⁶¹ Hapa, njoo, dada. Sikujui. Hatufahamiani, nadhani. Kama jambo hilo ni kweli... ili kwamba wasikilizaji waweze kuona ya kwamba hatufahamiani, unaona. Kama... Hii ni kama vile ambapo Bwana wetu alikutana na mwanamke siku moja. Na hapa tunakutana tena, tunakutana baada ya miaka elfu mbili juu ya ahadi Yake, na hawa hapa mwanamume na mwanamke wanakutana kwa njia ile ile. Sijapata kukuona maishani mwangu. Ninadhani sisi hatufahamiani, lakini Mungu anatumia sote wawili.

¹⁶² Sasa kama Roho Mtakatifu, Kristo aliye hapa ndani na ndani yako, atafunua umesimma hapa kwa sababu gani, ama jambo fulani kukuhusu wewe, je! ungejisikia una shauku kama yule mwanamke alivyokuwa siku ile? [Dada anasema, “Amina.”—Mh.] Sasa kilichokuleta hapa ni maombi, na maombi kwa ajili ya ugonjwa katika titi lako. Hiyo ni kweli. Kama jambo hilo

ni kweli, inua mkono wako. Sasa unaamini Mungu anaweza kuniambia ni titi gani? Ni titi la mkono wa kuume. Hiyo ni kweli.

¹⁶³ Watu wanaendelea kusema kule nje, mtu fulani aliingia, akisema, “Yeye anakisia jambo hilo.” Mimi silikisii. Msiwazie hivyo. Hilo linazuia, mnaona. Sasa kumbukeni, hamwezi kuficha mawazo yenu sasa. Naam. Hiyo ni kweli. Naam. Sawa.

¹⁶⁴ Hapa, unapaswa kuamini, wewe ni mhubiri, mhubiri mwanamke. Hiyo ni kweli, sivyo? Vema. Nenda, amini sasa, nawe utakuwa mzima. Mungu akubariki. Amini tu.

Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁶⁵ U hali gani? Sisi hatufahamiani. [Huyo dada anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Sikujui. [“La, bwana.”] Mungu anakujua. Kama jambo hilo ni kweli, inua mkono wako ili... Wewe ni mdogo sana kuliko mimi. Labda yule mwanamke aliyekutana na Bwana wetu alikuwa mdogo zaidi.

¹⁶⁶ Sasa mwanamke mwingine alisimama hapa. Mtu mwingine huko anaamini. Yule pale ameketi moja kwa moja pale. Ana shida ya kifua chake. Hiyo ni kweli? Uligusa vazi la nani? Lake. Imekwisha sasa. Yesu Kristo akufanya mzima.

¹⁶⁷ Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa mwanamke huyo yuko futi ishirini kutoka kwangu, lakini hakunigusa mimi. Alingusa Kuhani Mkuu. Hivi hamwoni, alikuwa nyuma yangu, inaonyesha ya kwamba ni Yeye Yule aliyefanya ile ahadi, yeye yule tu leo.

¹⁶⁸ Unaumwa ugonjwa wa neva, una wasiwasi sana, hasa sana jioni sana, unaninii, wakati unapokuwa umechoka na umedhoofika. Unawasiwasi sana. Halafu una sumu mwilini mwako. Inatia sumu damu yako. Lakini, hiyo ni kweli. Halafu una mzigo mkubwa sana juu ya mtu fulani apate kuokolewa, sivyo? [Dada anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Ndiyo, bwana, hiyo ni kweli. Unaamini sasa? [“Ndiyo.”] Vema, nenda. Kama vile ulivyoamini, na iwe kwako. Uwe na imani.

Usitilie shaka. Uwe na imani kwa Mungu. Amini tu.

¹⁶⁹ U hali gani, mama? Mimi ni mgeni kwako, nadhani. Kama jambo hilo ni kweli, basi tunainua mikono yetu, wapate kuona. Sijapata kumwona maishani mwangu.

¹⁷⁰ “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kama Bwana Yesu atamwambia mwanamke huyu, aliye papa hapa sasa, jambo fulani kumhusu, ambalo sijui kitu juu yake! Vema, sisi hatufahamiani, sisi, huyu mama anasimama hapa tu, mnaona. Vema, utaamini? [“Amina.”]

¹⁷¹ Una shida ya tumbo, linakusumbua, wewe unayeketi moja kwa moja hapo umevaa hilo koti jeusi. Hivi sasa linakusumbua. Kama jambo hilo ni kweli, inua mkono wako. Mnaona? Mnajua

kwa nini? Ni tumbo la mwanamke huyu, pia. Mnaona? Hiyo ni kweli.

¹⁷² Mnaona ule mwali mweusi unaowaunganisha pale? Ni ibilisi. Mnaona? Anajaribu kujificha, mnaona. Hawezi. Hawezi kujificha kwa Mungu. Hilo ni jambo moja la hakika. Tuko katika Uwepo wa Yesu Kristo. Hamna budi kuamini. Iweni na imani.

¹⁷³ Yeye alingusa nani? Hakunigusa mimi kamwe. Simjui mtu huyo. Hatufahamiani, bwana, sikujui wewe? Inua mkono wako kama jambo hilo ni kweli. Mnaona? Aligusa kitu gani? Yesu Kristo. Msikose kuona jambo fulani.

¹⁷⁴ Sasa huyu mama hapa. Naam. Loo, mama huyo amefunikwa na kivuli. Ni kifo juu yake. Anaumwa kansa, na kansa hiyo iko kwenye tumbo na pia kwenye utumbo mkubwa. Yeye, ndiyo kwanza wamkatie tamaa. Anakufa, kwa kansa. Hiyo ni kweli, siyo, mama? Hivyo ndivyo ulivyoambiwa. Sasa angalia hapa. Wewe, kuna tumaini moja tu ulilo nalo, hilo ni Kristo.

¹⁷⁵ Unaniamini mimi kuwa mtumishi Wake? Kitu fulani hakina budi kuniambia jambo hilo, sivyo? Kitu fulani hakina budi kuniambia. Mimi—mimi sininii, singelijua mimi mwenyewe. Nikikwambia wewe ni nani, utaamini mimi ni nabii Wake? Ingekusaidia? Ingekusaidia ama sivyo? Bibi. Crosley. [Huyo dada anasema, “Loo!”—Mh.] Basi rudi nyumbani.

¹⁷⁶ Mnaamini? Ni wangapi wenu sasa wanaamini kwa moyo wenu wote? Simameni kwa miguu yenu na mkubali jambo hilo. Simameni tu moja kwa moja, na kusema, “Ninaamini.” Inueni mikono yenu, kila mahali.

¹⁷⁷ Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, Ibilisi na nguvu zake zote na akemewe. Bwana Yesu Kristo, ambaye ameahidi jambo hili kwa ajili ya siku ya mwisho, Yeye yuko hapa sasa. Na iwe, Bwana, katika saa hii, ya kwamba watu hawatashindwa. Na waone kile Mungu anachotikisa mbele zao, kabla tu ya moto kushuka. Jalia kundi hili la Ibrahimu, huu Mzao kwa kifalme wa Ibrahimu, ufahamu saa tunayoishi! Ee Yesu, Mwana wa Mungu, mguse kila mtu aliye mgonjwa hapa. Waponye, Bwana. Namoba imani yao itambue ya kwamba wao wanasimama katika Uwepo wa Mungu aliyewaokoa na atakayewahukumu kwenye Siku ile. Naomba Nguvu Zake ziwashukie sasa, na kumponya kila mtu hapa aliye katika Uwepo wa Kiungu.



MABWANA, SISI TUNATAKA KUMWONA YESU SWA64-0304

(Sirs, We Would See Jesus)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marriion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumanne asubuhi, 4 Machi, 1964, katika Hekala la Bandari ya Nafsi kule Dallas, Texas, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1999 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1999 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org